31:1-34:12 SIKU ZA MWISHO ZA MUSA

Mipango kwa wakati wa usoni (31:1-29)

Musa alipojua kwamba siku za maisha yake hapa duniani zimebaki chache tu, aliukabidhi uongozi wa Israeli mkononi mwa yeye aliyechaguliwa na Mungu kuwa mfuasi wake, yaani Yoshua. AliwaonyaYoshua na watu pia kwamba, wangejitoa kwa wajibu uliowakabili bila hofu na kumtegemea Mungu kabisa, Yeye angewapa ushindi juu ya Wakanaani na kuwapa nchi ya ahadi (31:1-8,14,15,23; taz.maelezo ya Hes 27:12-23).

Kisha Musa alifanya mipango mitatu, watu wasije wakasahau wajibu wao wa agano. Kwanza, aliwaamuru makuhani wahakikishe kwamba sheria yote isomwe hadharani kila mwaka wa saba (9-15). Pili, yeye mwenyewe alitunga wimbo ambao watu wangeukumbuka kuwa onyo na kumbukumbu daima (16-23). (Wimbo huo umeandikwa katika fungu la 32.) Tatu, aliweka sheria yote, jinsi alivyokuwa ameiandika mwenyewe, katika sehemu ya usalama karibu na sanduku la agano, ili iwe ushahidi kwa Waisraeli, kama wangeiacha na kuasi. Nakala hiyo ya sheria yote iliyokuwa karibu na sanduku la agano, ilikuwa kumbukumbu na ushuhuda maalumu wa hali ya mambo yote ya maisha na uadilifu (24-29).

Mpango huu pia ulilingana na desturi za kale kuhusu agano baina ya mkuu na raia zake. Nakala ya agano ilitunzwa mahali patakatifu pa watu, na viongozi baada ya muda fulani walisoma sheria zake hadharani, ili kuwakumbusha watu wajibu wao kuhusu agano.

Wimbo wa Musa (31:30-32:47)

Musa akijua tabia ya watu ya kumwasi Mungu (taz.mst.29), aliwaachia wimbo aliotaka kila mtu autambue sana (30). Wimbo huo uliwakumbusha Waisraeli habari za upendo na utunzaji wa Mungu kwa ajili yao, na umuhimu wa kuwa waaminifu kwake. Ulieleza habari za wakati wa usoni na kukumbusha mambo yaliyopita: Katika haki yake, Mungu angewaadhibu, na katika neema yake, angewasamehe tena kama wangetubu.

Kama vile mvua inavyosaidia nyasi mbichi, maneno ya Musa yaliwasaidia Waisraeli (31:30-32:3). Mungu akiwa kama mwamba, aliwapa Waisraeli (Yeshuruni) ulinzi na kuwaimarisha. Akiwa Baba yao, aliwapa mahali pa heshima kati ya mataifa, na nchi ya Kanaani kuwa urithi wao. Lakini kwa njia ya ubishi na ubinafsi wao, waliharibika na kumwaibisha Baba yao (4-9). Aliwatunza kwa upendo na uangalifu, akiwapa yote waliyohitaji kwa maisha yao, lakini badala ya kumshukuru walimdharau tu. Badala ya kumwabudu waliabudu miungu ya kipagani (10-18). Kwa hiyo Mungu aliwaadhibu (19-25).

Lakini Mungu asingekubali Waisraeli waangamizwe kabisa, watu wengine wasije wakasema kwamba wao, wala siye Mungu, ni wenye nguvu juu ya Waisraeli na juu ya mambo yanayohusu uteuzi wao. Kama mataifa yale yangekuwa na ufahamu wo wote, yangetambua kwamba yasingekuwa na uwezo wo wote wa kuwashinda Waisraeli kwa njia ya ajabu namna hiyo, isipokuwa Mungu mwenyewe angewaruhusu (26-30). Mungu wa Waisraeli ni mwenye haki na mwenye nguvu. Miungu ya maadui ni waovu, wachafu, na wenye ukatili (31-33).

BWANA siku zote anaendelea kuwa mtawala na Mwenyezi. Yeye angetumia mataifa mengine ili kuwaadhibu watu wake, lakini angeyaadhibu mataifa hayo pamoja na miungu yao kwa ajili ya maovu yao. Kisha Waisraeli pia wangeona ubatili wa miungu isiyokuwa na nguvu. Wangemrudia BWANA, naye angewaponya tena (34-43).

Musa aliwaagiza watu wajifunze wimbo huo kwa moyo, nao wauimbe ili kujikumbusha sheria na kuitimiza, pia uwe onyo kwao juu ya mambo ya hatari ambayo yangetokea kama wangeasi. Lakini zaidi ya yote, sheria ilikusudiwa kuwa wema wa watu, ili waweze kuyafurahia maisha katika nchi waliyopewa na Mungu (44-47).

Baraka ya Musa (32:48-33:29)

Kama Mungu alivyotangaza hapo awali, wakati wa kufa kwake Musa uliwadia (48-52; taz.Hes 27:12-14). Katika mbaraka wa unabii aliowapa Waisraeli kabla ya kufa kwake, alitabiri majaliwa yote ambayo Mungu angewapa, kabila kwa kabila. Lakini kabla yake, Musa aliwakumbusha tena jinsi walivyopewa sheria katika Mlima Sinai. Mungu alitokea katika utukufu wa moto, akitoka katika utukufu uliokuwa mkubwa kuliko jua linapochomoza. Majeshi ya watumishi wa mbinguni yalikuwa pamoja naye, yaani wao wanaotimiza makusudi yake katika maisha ya watu binafsi na katika mataifa. Alikuwa Ndiye Aliye, Mfalme wa Israeli, ambaye alitoa sheria yake na kuwapa mkutano wa watu wake (33:1-5).

Kabila la Rubeni, ingawa lilipoteza haki yake ya mzaliwa wa kwanza, lisikubali kuwa dhaifu (6; lNya 5:1). Yuda lililokuwa kabila lenye nguvu zaidi. Licha ya kuhakikisha kuishi kwa usalama, pia lilitakiwa lisaidie makabila mengine, kama yangepata shida. (Kabila la Simeoni lisilotajwa hapa, baadaye liliingiliana kabisa katika kabila la Yuda)(7). Lawi, kabila la Musa na Haruni, lilikuwa na madaraka juu ya huduma yote ya kidini na kufundisha sheria. Watu wa kabila hilo walifaulu mtihani wa Mungu huko Masa, nao walithibitisha uaminifu wao kwa agano katika Mlima Sinai, lakini waliasi huko Meriba (8-11; taz.Kut 17:1-7; 32:25-29; Hes 20:10-13). (Kuhusu Thumimu na Urimu taz.maelezo ya Kut 28:15-30.)

Kabila la Benyamini lilipata baraka yake ya pekee baadaye, hekalu la Mungu lilipojengwa katika eneo la urithi wake, ingawa sehemu nyingine za mji wa Yerusalemu zilikuwa katika eneo la Yuda (12). Makabila mawili ya Yusufu, yaani Efraimu na Manase, yangerithi sehemu bora katika nchi ya

Kanaani. Mungu yule yule aliyemtokea Musa katika kichaka kilichowaka moto, angewapa nguvu ya pekee, ili hapo baadaye yawe makabila ya kuongoza katika ufalme wa kaskazini (13-17).

Zabuloni na Isakari yangefanikiwa kwa bidii yake ya biashara na utajiri wa ukulima uliokuwa alama ya eneo lake (18-19). Watu wa Gadi walichagua nchi yao mashariki mwa Yordani, lakini walitimiza ahadi yao ya kuwasaidia ndugu zao wa makabila mengine kwa kuteka nchi ya Kanaani. Walikuwa askari hodari sana kwa vita (20-21). Dani lingethibitisha kuwa kabila lenye hila (taz.Amu 18:1-31), lakini kabila la Naftali lingeridhika katika maisha ya utulivu katika nchi ya milima yenye rutuba nyingi karibu na Ziwa Galilaya. Kabila la Asheri lingeishi katika eneo lenye rutuba lililolindwa vizuri sana, ambalo mashamba yake yenye miti ya matunda yangetoa mafuta ya uto bora katika Palestina yote (22-25). Hali likilindwa na kubarikiwa na Mungu, taifa lote la Israeli lingefurahia ushindi, mafanikio na raha (26-29).

Kufa kwa Musa (34:1-12)

Kabla ya kufa kwake, Musa aliruhusiwa kukwea kilele cha Pisga cha Mlima Nebo katika eneo la Abiramu (karibu na marago ya Waisraeli yaliyokuwa tambarare za Moabu), ili aweze kuona uzuri na ukubwa wote wa nchi ambayo watu wake wangepata baada ya muda mfupi (34:1-4).

Sehemu maalumu ya kaburi la Musa haikujulikana (5-8). Yoshua alikuwa kiongozi mpya badala ya Musa, lakini Yoshua hakuwa na uwezo wa pekee kama Musa wala mtu mwingine baada yake, yaani wa kusema na Mungu ana kwa ana, na kujua mawazo yake na kutimiza matendo yake makuu (9-12).